**Learning by Ear – Hygiene: How to avoid diarrhoea**

**Episode 03** **"Kinachoua"**

**Author:** **Njoki C. Muhoho**

**Medical Advisor** **Dr Ng'ethe Muhoho**

**Editor** **Maja Braun**

**Kisuaheli** **Eric Ponda**

| Scene | Characters | | |
|---|---|---|---|
| **1** | 1. | MAMA SAM | |
| | 2. | CHEMU | |
| | 3. | NARRATOR | |
| | 4. | EDDI | |
| **2** | 1. | DR SALLY | **SAM – 17, m.** |
| | 2. | EDDI | **MAMA SAM – 40, f.** |
| | 3. | CHEMU | **MARIA – 43, f.** |
| | 4. | NARRATOR | **EDDI– 36, m.** |
| | 5. | MAMA SAM | |
| **3** | 1. | DR SALLY | **DR SALLY – 34, f.** |
| | 2. | MAMA SAM | **CHEMU – 15, f.** |
| | 3. | EDDI | |
| **4** | 1. | CHEMU | **ANNOUNCER – m.** |
| | 2. | DR SALLY | **NARRATOR** |
| | 3. | NARRATOR | |
| | 4. | ANNOUNCER | |
| **5** | 1 | EDDI | |
| | 2 | CHEMU | |
| | 3 | DR SALLY | |
| | 4 | MAMA SAM | |
| | 5 | NARRATOR | |

**INTRO**

**MUSIC: THEME MUSIC**

**01. NARRATOR** **Hujambo na karibu kwa sehemu ya tatu ya mfululizo wa vipindi vya LEARNING BY EAR NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO tukiwa bado kwenye masuala ya Usafi na kinga dhidi ya ugonjwa wa Kuhara. Katika makala iliyotangulia, Mtoto Fatu ambaye amekuwa akihara anapelekwa hospitalini na Mjomba Eddi,afisa wa huduma za Afya ya jamii ambaye pia ni shemejiye Mjane Mama Fatu.Sam Kakake mkubwa Fatu, bado hajapata nafuu baada ya kuugua maradhi haya ya kuhara.** .

Je Mtoto Fatu atapona?.Hebu tuungane na Eddi na Familia nzima katika Hospitali ya sehemu hiyo.

Endelea kutusikiliza ili ujifunze mengi kuhusu kinachosababisha Kuhara, jinsi ya kutibu na kinga dhidi ya ugonjwa huu, katika hadhithi hii inayomhusu Sam, Familia na Marafiki zake.

**SCENE 1: HOSPITAL TRIAGE UNIT**

**02.** ***SFX: BABY CRIES, BACKGROUND SIRENS, HOSPITAL NOISES ETC. AND FAR AWAY SOUNDS OF AMBULANCE AND CRACKING INTERCOMS***

**03. MAMA SAM :** ***(silently crying)*** Nusra nimuue Mwanangu…! Sijui ningefanyaje kama ningempoteza mwengine wa Familia yetu. Kwanza Baba Sam, kisha sasa

nimpoteze Mtoto wangu Fatu…! hhhe ..Eddi nifanyeje sasa….?

**04. EDDI :** **Mama Sama kuwa na subra, wanajaribu kumfanyia uchunguzi.**

**05. MAMA SAM :** **Uchunguzi wa nini? Kwanini wasimpe tu Dawa na kuturuhusu kurudi nyumbani?**

**06. EDDI :** **Kwanza ni lazima wampime ndipo wajue Mtoto Fatu ameambukizwa aina gani ya vidudu au vimelea ndipo waweze kumpa dawa mujarab.**

**07. MAMA SAM :** **Unamaa kuwa zile ndizi za jivu zilizotayarishwa na Maria kamwe hazingeweza kumsaidia au kumponya binti wangu?**

**08. EDDI :** **Fatu alipasa kuletwa Hospitalini katika siku saba za mwanzo baada ya kuanza dalili za kuhara. Ugonjwa wa kuhara ni hatari sana, na unapasa kutibiwa haraka iwezekanavyo. Ndizi zile zinaweza kuwa dawa kwa maradhi mengine ila sio ugonjwa huu wa kuhara.**

**09. MAMA SAM :** Lakini rafiki yangu Maria amejitolea kwa hali zote zile. Amekuwa akifanya kila juhudi kuyaokoa maisha ya Mtoto wangu Fatu . Oooh mwanangu Chemu najua Mamako alikuwa na nia njema!.

**10. CHEMU :** **Mungu amsaidie Fatu…!**

**11. EDDI :** **Madaktari pia ni lazima wachunguze athari zilizosababishwa na viini vya maradhi haya.**

12. **MAMA SAM ; Maskini Mtoto wangu….! Najutia matendo yangu..!.**

13. **EDDI :** Sshhhh usisema hivyo..! Wewe ni mama mzuri sana , ni vile tu hukufahamu mengi kuhusu ugonjwa huu wa kuhara ili uweze kuwakinga wanao.

14. **MAMA SAM ; Lakini viini hivi vilitokea wapi? Mimi sifugi viini vyovyote nyumbani kwangu.**

15. **EDDI :** *(chuckles sadly)* Viini hivi viko kila mahali Mama Sam..!

16. **CHEMU : Viko kwenye mikono yetu… ! Mwalimu hutuambia kila mara kwamba tusiponawa mikono tunaweza kuambukizwa ugonjwa huu wa kuhara. Mama Sam, nilikwambia tuwe tukinawa mikono yetu lakini akanipuuza….**

17. **EDDIE ;** Chemu, tutazungumza mambo hayo baadaye, sio sasa …!, nadhani madaktari wako tayari hebu sasa twendeni tukawaone! Tunabahati mke wangu ndiye anayeshika zamu leo.!.

**BRIDGE MUSIC**

**<u>SCENE 2: DR SALLY'S OFFICE</u>**

18. ***SFX: FOOTSTEPS APPROACHING*.**

19. **MAMA SAM :** Dkt Sally, Dkt Sally Tafadhali nieleze Mtoto wangu atapona.,…! atapona sivyo?

**20.** **DR. SALLY** **:** Fatu anaendelea kupata matibabu, lakini…hali yake si nzuri sana vile kwa kweli. Kwanini hamkumleta mapema hospitalini?

**21.** **CHEMU** **:** Shangazi Sally, hawakutaka kunisikiza. Niliwambia kwamba Mwalimu alisema…

**22.** **EDDI** **;** Ngoja kidogo Chemu… subiri sio wakati huu.., hebu tumsikilize Daktari Sally anayapi …..!

**23.** **DR SALLY** **:** Fatu yuko hali mbaya sana, ameishiwa na maji mwilini na tumelazimika kumpeleka katika chumba cha wagonjwa mahututi..

**24.** **MAMA SAM** **:** Oh, Mungu wangu, kwahiyo siwezi kumuona….? Siwezi kumuona sasa sivyo..?

**BRIDGE MUSIC**

**<u>SCENE 3: PAEDIATRICS ICU</u>**

**25.** ***SFX: BABY CRIES. ICU MACHINES BEEPS***

**26.** **EDDI** **:** **Yule pale pembeni kwenye kile kitanda kidogo!**

**27.** **MAMA SAM** **:** Oooh Mungu wangu..!, kwani wamemfanyia nini?, Hhee wamemfanya nini? Amewekwa mipira kama …! sasa wanafanyia nini?

**28.** **EDDI** **:** Sssshhhh….. usiwe na wasi wasi..! ni lazima wamweke dawa na maji kwenye mishipa yake.

**29.** **MAMA SAM** **:** ***(crying)*** Eddi, Namtaka mwanangu! Nataka mwanangu apone… Nataka kumbeba mtoto wangu… tafadhali, tafadhali, tumpeleke nyumbani, nakuahidi nitamtunza, hilo nakuhakikishia Eddi…!

30. **EDDI** : ***(firmly)*** Hapa ndipo mahali panapomfaa huyu Mtoto. Hapa hapa Hospitalini..!

31. **NARRATOR** **Mama Sam anaketi kando kidogo tu ya kitanda cha Mtoto wake Fatu, akiwa na matumaini kwamba mwanawe atapona. Wakati huo huo, wakiwa katika chumba cha wageni, Chemu apata fursa ya kujifunza mengi kuhusu yale aliyoyaona katika wodi ya watoto hospitalini humo .**

## SCENE 4: HOSPITAL WAITING ROOM

32. ***SFX: FAR AWAY SOUNDS OF AMBULANCE AND INTERCOMS***

33. **CHEMU** : **Shangazi Sally, Mjomba Eddi na Mama Sam wameenda kumuona Fatu**!

34. **DR SALLY** : Ndio wameenda kumuona. Lakini yuko hali mbaya sana. Labda utamuona baadaye sio sasa..

35. **CHEMU** : Shangazi Sally?

36. **DR SALLY** : Naam Chemu?

37. **CHEMU** : Nimewasikia wakisema kuwa amewekwa ***Drip?.*** Nini maana ya ***Drip?***

38. **DR SALLY** : Chemu, Wakati mwengine tunapokuwa wagonjwa sana, kama vile ugonjwa wa kuhara, hupoteza kiasi kikubwa cha maji mwilini. Kama unavyofahamu sehemu kubwa ya mwili wa mwanadamu ni maji tu. Kwa hivyo tunapopoteza kiasi kikubwa cha maji haya, mwili unashindwa kufanya kazi kama inavyostahili. Ni

sawa na Gari lililoishiwa mafuta. Kwa hiyo ni lazima kuusaidia mwili kurudisha maji hayo yaliyopotea. Madaktari humuongezea mgonjwa maji mwilini kwa kumtia mipira ya kusambazia maji hayo.Hicho ndicho kinachotendeka kwa sasa..

**39.** **CHEMU** **:** Lakini kwanini asinyweshwe maji mengi tu kwa kikombe ?

**40.** **DR SALLY** **;** Haya si maji ya kawaida anayotiwa Mtoto Fatu.. Maji hayo yamechanganywa na dawa na chembe chembe za lishe bora.Unajua si tuu Fatu alikuwa anahara , bali pia alikuwa hali vizuri?

**41.** **CHEMU** **:** Oh, alikuwa akilia tu ….heee, heeee….! Heee….! kisha alale na akiamka kazi ni hiyo ya kulia….. hee…. hee ….hee…!

**42.** **DR SALLY** **:** Unaona, kwa hiyo anahitaji chakula pia. Anahitaji nguvu na lishe bora mbali na dawa za kuuwa viini na vimelea mwilini mwake.. Kwa sababu chakula hakiwezi kudumu kwa muda mrefu mwilini, ni lazima tutafute njia za kuhakikisha kuwa chakula hicho kinaingia kwenye mishipa ili kumpa nguvu zaidi.Ndio sababu tunatumia mipira kukisambaza chakula kwenye mishipa yake moja kwa moja.

**43.** **CHEMU** **:** Shangazi Sally,wewe ni mwerevu sana . Pia mimi ningependa kuwa daktari kama wewe. Nataka ku….

**44.** ***SFX: A RUSH OF FOOTSTEPS TOWARDS THEM***

**45. MAMA SAM :** **(Crying loudly)** SALLY….. Sally… Sally… Njoo… njoo upesi, mtoto wangu anakufa… njo … njoo upesi…!

**46. CHEMU :** Ni nini…kumetokea nini…..?

**47. EDDI :** Sally, njoo huku upesi, upesi mwanangu Fatu yuko hali mahututi, amezidiwa….!

**48.** ***SFX: INTERCOM CRACKS TO LIFE.***

**49. HOSPITAL ANNOUNCER/INTERCOM** Daktari Sally Mwanka…! Daktari Sally Mwanka……!, Tafadhali unahitajika upesi katika wodi ya watoto….! Daktari Sally Mwanka tafadhali fika upesi katika wodi ya watoto.

**50.** ***SFX. MANY FOOTSTEPS RUSH AWAY***

**BRIDGE MUSIC OF SAD NATURE**

**51. NARRATOR** UGONJWA WA KUHARA UMEMUUA MTOTO MWENGINE BARANI AFRICA.FATU SASA NI MMOJA WA WATOTO WANAOFARIKI KUTOKANA NA UGONJWA HUU. UGONJWA WA KUHARA NI TISHIO KUBWA NA HUCHANGIA PAKUBWA KUSABABISHA VIFO VINGI MIONGONI MWA WATOTO BARANI AFRICA LICHA YA KWAMBA UNAWEZA UKAZUIWA..

**<u>SCENE 5: DR SALLY'S OFFICE</u>**

**52. CHEMU :** (***Crying)*** Fatu amefariki…..siamini…siamini kabisa….!

**53. MAMA SAM :** ***(whim pering)*** **Yote haya ni kwa sababu yangu. Ni makosa yangu. Nilipasa kuchukua hatua za haraka**

**na mapema. Sasa nimesababisha kifo kingine katika familia yangu..**

54. **EDDI** : **Pole,…! pole….! pole dadangu,** … hayo ndiyo hali ya dunia, Mwenyezi Mungu ametoa na akatwaa.

55. **CHEMU** ; (***sniffling***) … Inahuzunisha. Yeye ndiye mpaji, na mwenye uwezo wa kuchukua ?. Mbona hangeuchukua ugonjwa huu wa kuhara. Kwanini hangeweza kutuondolea ugonjwa jamani na kumnusuru Fatu wetu? *(**cries**).*

56. **DR SALLY** : Mama Sam, Tumejaribu kadri ya uwezo wetu lakini Mungu amemchukua…..!.Natamani ningekuwa na uwezo wa kubadili mambo. ……! Tumechelewa. Ningejua mapema kuhusu ugonjwa wa Fatu…..!

57. **CHEMU** : *(**angry**)* Kifo jamani hakina huruma… Hakina huruma kabisa … sasa tutamlea nani?

58. **DR SALLY** : Ningekuwa namtembela mara kwa mara. Angalau ningeweza….

59. **EDDI** : Sally, tafadhali si makosa yako. Mimi ndiye nilipasa kuwa nawatembelea mara kwa mara. Wewe ni mjane wa marehemu Kakangu ..! Na ninawajibu wa kukuangalia vizuri. Nina jukumu la kukujulia hali mara kwa kwa mara ili kuwa karibu nanyi zaidi

60. **CHEMU** : ***(screams suddenly)*** Ooh oohhh nafa…..! nafaa..! … jamani nafa, shangazi Sally nisaidie…. Nafa… tafadhali nisaidie

61. **EDDI** : **Nyanmaza, nyamaza Chemu** !

62. **DR SALLY** : ***(alarmed)*** Chemu, kwanini unasema unakufa?

**63. CHEMU ; Nimemgusa Fatu, na sijanawa mikono, Mwalimu alisema*……(stops)***

**64. DR SALLY : Mwalimu alisema nini** ?

**65. CHEMU : Yamo kwenye huu wimbo!**

***(rapping)*** Osha mikono yako,Osha mikono yako
***Mikono safi tu,itumiwe kwa kula***
***Wasiojali tu hutumia mikono michafu***
***Baada ya msala,Osha mikono yako***
***Dumisha afya yako,Osha mikono yako***

**66. DR SALLY Sikiliza hapa Chemu. Huo wimbo ni mzuri. Unapasa kuwafunza watoto wengine hapa kijijini. Sasa nenda ukaoshe mikono kwenye kile kijibeseni pale na uache kulia. Hutakufa….!. Mimi niko hapa na wewe.. Mimi ni shangazi yako na kisha Daktari. sawa.?**

**67. MAMA SAM** *(**wailing**)* Mtoto wangu ametuacha , mwanangu ameaga

**68. CHEMU :** *(**in shock**)* Sam!!!!

**69. EDDI : Sasa ni nini**? Sam ana nini ?

**70. CHEMU ;** Sam!!! Sam!!!......Anakufa… atakufa...ohh ooh maskini Sam … Sam!!.. Hapana sio Sam…..

**71. DR SALLY :** *(**interrupts**)* Chemu… unamaanisha nini… eti nini ?…Sam yuko wapi?

**72. MAMA SAM :** ***(wailing)*** Mungu nihurumie …. Nuhurumie….munusuru Mwanangu Sam… Akifa mimi nitabaki na nani…? Watu wote wanafariki katika nyumba hii. Mungu pia mimi nichukue…...pia mimi nichukue..!. Nipe ugonjwa huu wa kuhara pia nife…. niweze kuungana na watoto wangu…..! Baba Sam……… niko njiani naja ***(wails more).***

**73. EDDI ;** Chemu, wacha kulia …. Hebu tueleze kuhusu Sam. Sam ana nini, yuko wapi, hheee….ana nini ?

**74. CHEMU ;** Sam.. Sam.. yuko taabani …….kitandani… huko nyumbani… pia yeye kutokana na ugonjwa huu wa kuhara….

**75. DR SALLY :** He hee hee Eddi ingia ndani ya gari upesi…. twende…!

**76. MAMA SAM :** ***(wailing)…*** Oooiiii… oiiiii, Shetani amenivamia nyumbani kwangu…..! Ugonjwa wa Kuhara….pepo …! nenda kabisa wewe ni muuaji…,

**77. DR SALLY** Pole….. Pole…..! Mama Sam sasa twende nyumbani…!

**78. MAMA SAM** Siwezi kumuacha Mtoto wangu Fatu… lakini pia namhitaji Sam… siwezi kwenda… ! sasa nitafanya nini mimi….l ***(cries).***

**79. DR SALLY** Fatu yuko mikononi mwa hospitali.Mwili wake utahifadhiwa vyema tu hadi wakati wa maziko.. Lazima turudi nyumbani tukajaribu kuokoa Maisha ya Sam…! Tafadhali twende.. Twende….tafadhali Mama Sam …. Lazime tumlete Sam Hospitalini kabla mambo hayajaharibika.

**BRIDGE MUSIC – FAST PACED**

**<u>OUTRO</u>:**

**80. NARRATOR** MASKINI MAMA SAM. DUNIA IMEMGEUKIA. MAMBO YANAMWENDEA KOMBO.LAKINI CHA MSINGI SASA NI KUOKOA MAISHA YA WALIOSALIA KWA KUWAPELEKA HOSPITALINI KISHA KUCHUKUA MWILI WA MAREHEMU FATU KWA MAZIKO. KWA MARA NYINGINE BARA LA AFRIKA LIMEMPOTEZA MTOTO MWENGINE FATU.

KADHALIKA MAISHA YA VIJANA BARO BARO PIA YAMO HATARINI. NA HALI HIYO HAIPASI KUPUUZWA. SAM LAZIMA APELEKWE HOSPITALINI HARAKA IWEZEKANAVYO.

HADI HAPO TUNAFIKA MWISHO WA MAKALA HAYA, TUKITUMAI UTAUNGANA NASI WAKATI MWENGINE KWA MAKALA MENGINE YA MFULULIZO WA VIPINDI VYA NOA BONGO TUKIZUNGUMNZIA USAFI.KWA MENGI ZAIDI UNGANA NASI WAKATI MWENGINE UFAHAMU YATAKAYOMPATA SAM.

UKIPENDA KUSIKILIZA TENA MAKALA HAYA AU VIPINDI VYENGINE VYA NOA BONGO TAZAMA MTANDAO WETU WA www.dw-world.de/lbe NA IWAPO UNA MAONI PIA USISITE KUWASILIANA NASI. HADI WAKATI MWENGINE KWAHERI KWA SASA.